# MWONGOZO WA WANATAALUMA WA CKD KUJISAJILI NA KUMALIZA MASOMO YA SHAHADA ZA UZAMILI

***[kama ulivyoidhinishwa na Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) katika mkutano wake wa 257 uliofanyika tarehe 18 Septemba, 2019]***

## 1. KUJISAJILI

1.1 Mwanataaluma atakayeajiriwa katika cheo cha Mkufunzi Msaidizi (Tutorial Assistant) atatakiwa kujisajili katika masomo ya shahada ya umahiri ndani ya miaka miwili (2) tangu tarehe ya kuajiriwa na endapo atashindwa kujisajili katika kipindi hicho bila sababu za msingi atabadilishwa kada kuwa mfanyakazi mwendeshaji au atarudishwa Ofisi ya Rais Utumishi ili apangiwe kazi katika taasisi nyingine ya umma.

1.2 Mwanataaluma atakayeajiriwa na au kupandishwa daraja na kuwa na cheo cha Mhadhiri Msaidizi (Assistant Lecturer) atatakiwa kujisajili katika masomo ya shahada ya Uzamivu ndani ya miaka mitatu (3) tangu tarehe ya kuajiriwa au ya kupandishwa cheo kuwa Mhadhiri Msaidizi. Endapo atashindwa kujisajili katika kipindi hicho bila sababu za msingi atabadilishwa kada kuwa mfanyakazi mwendeshaji au atarudishwa Ofisi ya Rais Utumishi ili apangiwe kazi katika taasisi nyingine ya umma.

## 2. KUMALIZA MASOMO

2.1 Mwanataaluma atakayejiunga na masomo ya shahada ya umahiri na kuhitaji nyongeza ya likizo ya masomo ataongezewa likizo hiyo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja (1) tangu kuisha kwa likizo ya masomo aliyokuwa amepewa awali bila gharama yoyote ya nyongeza kwa upande wa CKD. Endapo atashindwa kumaliza masomo ndani ya muda huo wa mwaka mmoja wa nyongeza bila sababu za msingi mwanataaluma huyu atatakiwa kuripoti katika kituo cha kazi mara moja na atabadilishwa kada kuwa mfanyakazi mwendeshaji au atarudishwa Ofisi ya Rais Utumishi ili apangiwe kazi katika taasisi nyingine ya umma. Hata hivyo, kama atakaidi agizo la kuripoti katika kituo cha kazi atasimamishiwa mshahara mara moja na kuchukuliwa hatua nyingine za kinidhamu.

2.2 Mwanataaluma atakayejiunga na masomo ya shahada ya uzamivu na kuhitaji nyongeza ya likizo ya masomo ataongezewa likizo hiyo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili (2) tangu kuisha kwa likizo ya masomo aliyokuwa amepewa awali bila gharama yoyote ya nyongeza kwa upande wa CKD. Endapo atashindwa kumaliza masomo ndani ya muda huo wa miaka miwili ya nyongeza bila sababu za msingi mwanataaluma huyu atatakiwa kuripoti katika kituo cha kazi mara moja na atabadilishwa kada kuwa mfanyakazi mwendeshaji au atarudishwa Ofisi ya Rais Utumishi ili apangiwe kazi katika taasisi nyingine ya umma. Hata hivyo, kama atakaidi agizo la kuripoti katika kituo cha kazi atasimamishiwa mshahara mara moja na kuchukuliwa hatua nyingine za kinidhamu.